




Ada anacheka kwa
sababu
alisikia hadithi ya
kuchekesha.

Anatabasamu.

Ada anahisi nini?



Tisa anahisi hasira.

Ana mkunjo kipajini
kwake.

Kwa
nini amekasirika?



Yadoo anaogopa
giza.

Kila mtu huhisi hofu
wakati mwingine.

Lakini Yadoo
anaweza kuomba
msaada.



Chidu ana wasiwasi
juu ya kazi yake ya
shule.

Anaweza
kumwambia
mwalimu wake.

Anaweza kuomba
msaada.



Lushan anacheza
cheza!

Ni sawa kufanya
mchezo wakati
mwingine.



Ethuro anajisikia
mwenye huzuni.

Ni sawa kulia.

Hisia huja na
kwenda.



Yatoo amejawa na
furaha.

Yeye amefurahi.

Hisia huja na
kwenda.



Hadiza anahisi uvivu.
Anahitaji kupata kitu
cha kufanya.



Ayoo ana hasira.
Amechanganyikiwa.
Hasira ni hisia
ngumu.



Lizy amesisimka.

Je! Ni nini sababu ya
msisimko wake?

Mama alitayarisha
chakula
akipendacho.



Zege alihisi usingizi.

Alikuwa amechoka
sana.

"Lakini, 'kuhisi
usingizi' ni hisia?"
Effy anauliza.



Effy
amechanganyikiwa!

Je! Unaweza kujibu
swali lake?

A colorful illustration of a round character with dark curly hair. The character has large, expressive eyes and a small, open mouth. A pink speech bubble is positioned above the character's head. The background is white with several stylized, red and brown cloud-like shapes.

Lempaa anahisi
mshangao na
mshtuko.

Alisikia uvumi fulani.
Ni ukweli?



Nelly ni mgonjwa.

Anahisi huzuni.

Anahitaji dawa na
kupumzika ili ajisikie
bora.



Selina anahisi
kutosheka.

Amemaliza kazi zake
za nyumbani.

Sasa anaweza
kucheza.



Victor hana kazi leo.

Anamwonyesha
Selina vidole viwili.

"Kazi nzuri, sasa
hebu tucheze!"
anasema.